

HIGH STRATEGIES EXAM SERIES

DARASALATANO - MWISHO WA MUHULA WA KWANZA - 2020

KISWAHILI: LUGHA

Muda: Saa 1 Dak. 40

Chagua neno lifaalo kujazia mianya iliyoachwa wazi kutoka swali la 1 - 15.

Wanyapori ____ 1 ____ wanyama wanaoishi ____ 2 ____ . Nchi ____ 3 ____ ina mapori
____ 4 ____ yaliyo na wanyama ____ 5 ____ sana. Watalii wanapozuru ____ 6 ____ yetu au
wanapotembelea ____ 7 ____ yetu kuja kuwaona wanyama ____ 8 ____ porini hulipa ____ 9 ____
nyingi sana. Pesa ____ 10 ____ husaidia ____ 11 ____ kuleta maendeleo ____ 12 ____ nchi yetu.
Unawajua ____ 13 ____ wangapi? Unajua kwamba ____ 14 ____ wanyamapori wakubwa na
____ 15 ____ wadogo?

- | | | | | |
|-----|------------------|------------|------------------|----------------|
| 1. | A. ni | B. na | C. la | D. ya |
| 2. | A. porini | B. mbugani | C. bustanini | D. msituni |
| 3. | A. yetu | B. letu | C. zetu | D. petu |
| 4. | A. wengi | B. mengi | C. mingi | D. nyingi |
| 5. | A. mengi | B. wengi | C. mingi | D. mingi |
| 6. | A. inchi | B. nchi | C. nchini | D. inchini |
| 7. | A. pahali | B. eneo | C. maeneo | D. mahali |
| 8. | A. lao | B. hawa | C. hao | D. kwao |
| 9. | A. mapeni | B. mahela | C. pesa | D. mapesa |
| 10. | A. hio | B. nayo | C. hizi | D. hizo |
| 11. | A. kuwa | B. kua | C. kwa | D. katika |
| 12. | A. mwa | B. pa | C. la | D. ya |
| 13. | A. wanyamaporini | B. mapori | C. wanyamaporini | D. wanyamapori |
| 14. | A. kunako | B. kunayo | C. kuna | D. kunazo |
| 15. | A. mengine | B. wengine | C. zingine | D. vingine |

Tumia "ingine" kukamilisha sentensi zifuatazo.

16. Sitaki kitabu _____
A. kingine B. zingine
C. vingine D. mengine
17. Gari _____ limewasili na wanafunzi
A. lingine B. jingine
C. kingine D. mengine
18. **Kanusha sentensi hii**
Baba atakamua ng'ombe
A. Baba hakamui ng'ombe
B. Baba hajakamua ng'ombe
C. Baba hatakamua ng'ombe
D. Baba asikamue ng'ombe
19. **Kanusha sentensi hii:**
Mwalimu ametufundisha kiswahili
A. Mwalimu hatafundishi kiswahili
B. Mwalimu hatafundisha kiswahili
C. Mwalimu hajatufundisha kiswahili
D. Walimu hawajafundisha kiswahili


Chagua jibu sahihi

20. Watoto _____ wamo darasani
A. yote
B. wowote
C. wote
D. zote
21. Sitaki mzaha _____ hapa
A. yoyote
B. yeyote
C. zozote
D. wowote
22. **Andika wingi wa**
Kisu kimenolewa leo
A. Visu zimenolewa leo
B. Visu vitanolewa leo
C. Visu vimenolewa leo
D. Visu havijanolewa leo

Tumia 'ingi' kwa usahihi


23. Baada ya kukimbia Jeremia alilowa jasho _____
A. jingi B. mingi
C. mengi D. nyingi

24. Kuna maji _____ chunguni.
A. mengi B. nyingi
C. mingi D. jingi
25. Nomino samaki hupatikana katika ngeli gani?
A. KI - VI B. A - WA
C. LI - YA D. U - U
26. **Tegua kitendawili hili**
Nanywa supu, nyama natupa _____
A. firigisi B. papai
C. muwa D. kuku
27. Njunge alimuaga dada yake alamsiki, naye dada yake akamjibu binuru. Ilikuwa wakati gani?
A. Jioni B. Mchana
C. Asubuhi D. Usiku
28. Kiyoyo ni kwa bata naye ndama ni kwa
A. simba B. mbuzi
C. kondoo D. ng'ombe
29. Vazi hili ni



- A. gagro B. singeliti
C. kofia D. koti

30. Kati ya vifaa hivi ni kipi hakitumiwi na seremala?



- C.  D. 

Soma barua hii kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.

Shule ya msingi ya koko,
S.L.P 433,
Korokoroni.
3/05/2017.

Kwa mpendwa Baba,

U hali gani? Pokea salamu kutoka kwa mwanao Ema. Natumai u mzima na unachapa kazi vilivyo. Baba, nilipofunga shule muhula wa kwanza, nilifurahi kuwa nambari tatu kati ya watoto tisini na wawili. Nilikuwa na alama mia nne na tano, upinzani ulikuwa mkali mno. Kwani aliyenishinda alikuwa na alama mbili tu mbele yangu.

Watoto wameongezeka sana. Tuko wengi darasani kuliko tulivyokuwemo katika darasa la nne. Somo ambalo lilinitoa jasho ni Kiswahili. Kuliimarisha somo hili naomba uninunulie kitabu cha *kurunzi ya Kiswahili*.

Nakushukuru Baba kwa upendo wako kwangu. Mama na kaka yangu Nyandeké wanaendelea vizuri huku nyumbani.

Kwaheri.

Ndimi Bintiyo
Ema Thiodora

- | | |
|---|---|
| <p>31. Mwandishi anasomea shule gani?
A. Shule ya Msingi ya Koko
B. Shule ya Korokoroni
C. Chuo cha Koko
D. Anwani ya Koko</p> <p>32. Mwandishi hupata barua yake wapi?
A. Kwenye posta ya Korokoroni
B. Kwenye posta ya Koko
C. Kwenye posta ya Ukwala
D. Kwenye posta ya Kiambu</p> <p>33. Barua hii iliandikwa lini?
A. 4/3/2017
B. 3/4/2017
C. 3/05/2017
D. 05/3/2017</p> <p>34. Mpokeaji wa barua hii ni
A. Ema
B. Koko
C. Thiodora
D. Baba</p> <p>35. Kutokana na barua hii, mwandishi yumo katika darasa la _____
A. nne
B. sita
C. tano
D. saba</p> | <p>36. Aliyemshinda mwandishi alikuwa na alama ngapi?
A. 405
B. 407
C. 402
D. 704</p> <p>37. Kuna watoto ngapi kwenye darasa la kina mwandishi?
A. 92
B. 62
C. 29
D. 26</p> <p>38. Ni somo lipi mwandishi hakulifanya vizuri?
A. Kiswahili
B. Hisabati
C. Sayansi
D. Dini</p> <p>39. Mwandishi anashukuru Babake kwa _____
A. ukarimu wake
B. upendo wake
C. umoja wake
D. kazi yake</p> <p>40. Ni nani aliyeiandika barua hii?
A. Baba
B. Mama
C. Thiodora
D. Nyandeké</p> |
|---|---|

Soma hadithi hii kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.

Tumerudi tena shuleni kwa muhula mwingine. Tuna matumaini kuwa tutasoma salama salimini. Tunawashukuru walimu wetu waliotufundisha mambo mengi. Tulijifunza salamu adabu na heshima. Tuna adabu kwa wakubwa na wadogo. Tunawasalimia wakubwa wote "shikamoo" na tunaheshimiana na vijana wenzetu. Tunatumia lugha za adabu. Tunasema, "ninaomba, tafadhali, samahani, pole na asante."

Tumejifunza vitendawili, hadithi, mashairi nyimbo, methali na mafumbo. Tumeandika na tutaendelea kuandika insha kwa hati nadhifu na imla pia. Tumesoma na tutasoma ngeli pamoja na viashiria, viulizi, vimilikishi vikanushi na vivumishi vyote. Jamani wanafunzi wenzangu tumakinike kwani walimu na wazazi wetu wako tayari kutupiga jeki hivi karibuni katika muhula huu wa pili. Wote wanataka tufaulu masomoni kisha maishani.

- | | |
|---|--|
| <p>41. Kauli "Tumerudi tena" inamaanisha kuwa
A. wanafunzi walikuwa likizoni
B. wanafunzi walienda matembezi
C. wanafunzi walienda harusini
D. wanafunzi walienda michezoni</p> <p>42. Wanafunzi watasomaje muhula huu?
A. Salama sana
B. Salama salimini
C. Salimini tu
D. Kwa huzuni</p> <p>43. Walimu wamepewa shukrani kwa sababu gani?
A. Hawakuwafundisha mambo mengi
B. Walijaribu kuwafundisha
C. Waliwafundisha mambo mengi
D. Walitamani kuwafundisha</p> <p>44. Watoto walijifundisha mambo haya yote shuleni isipokuwa
A. salamu na adabu
B. vitendawili na hadithi
C. ukulima na uchimbaji
D. methali na mafumbo</p> <p>45. Salamu ya wadogo kwa wakubwa ni gani anavyosema mwandishi?
A. Mambo
B. Ni aje
C. Sasa buda
D. Shikamoo</p> | <p>46. Mwandishi anawahimiza wanafunzi wenzake wafanye nini?
A. wasisome hadithi
B. wasiwe na adabu
C. wamakinike kimasomo
D. wawe watoro shuleni</p> <p>47. Ni ipi siyo lugha ya adabu asemavyo mwandishi
A. tafadhali
B. samahani
C. asante
D. nataka</p> <p>48. Jibu la salamu <i>shikamoo</i> ni
A. marahaba
B. shikamoo sana
C. asante sana
D. karibu</p> <p>49. Wanafunzi waliandikaje insha?
A. Kwa udhaifu
B. Kwa unyonge
C. kwa hati nadhifu
D. kwa uvivu</p> <p>50. Hadithi hii inaweza kuelezwa wapi?
A. Nyumbani.
B. Hospitalini.
C. Shambani.
D. Shuleni.</p> |
|---|--|